

## BENK YA AZANIA YAZINDUA HATIFUNGANI YA "BONDI YANGU" KATIKA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM



**24.01.2025:** Benki ya Azania kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam leo imezindua hatifungani yake ya "Bondi Yangu" yenye thamani ya **shilingi bilioni 30 (TSH. 30,000,000,000)** na uwezekano wa kuchukua ziada ya shilingi bilioni 15 (TSH. 15,000,000,000), ikiwa ni toleo la kwanza la programu ya hatifungani ya Azania yenye thamani ya shilingi za kitanzania Bllioni Mia Moja (TSH. 100,000,000,000).

### MATOKEO YA MAUZO YA HATIFUNGANI

Mauzo ya hatifungani ya Azania yalifunguliwa tarehe 04 Novemba 2024 na kufungwa tarehe 06 Desemba 2024, ambapo kiasi cha shilingi 63,267,980,000 kimepatikana ikilinganishwa na shilingi bilioni 30 zilizotarajiwa kukusanywa, sawa na mafanikio ya asilimia 210.9.

**Mgeni Rasmi** wa tukio hili alikua ni **Waziri wa Fedha Mh.Dk. Mwigulu Nchemba (Mb)**, akisondikizwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) CPA. Nicodemus Mkama , Afisa Mtendanji Mkuu wa Soko la Hisa la Dar es salaam Ndg. Peter Nalitolela na Mkurugenzi na Mkurugenzi Mkuu wa Azania Bank Plc Bi. Esther Mang'anya.